

Saint Camillus
Pray for us

By Fr. Evans Juma M.I.

# Feast of Saint Camillus de Lellis, Camillians Kenya Family Day

&

Temporal Profession

of



**Nov. Innocent Moindi**
(TABAKA PARISH-KISII DIOCESE)



**Nov. Adrian Sagwe**
(SUNEKA PARISH-KISII DIOCESE)



**Nov. Boniface Kioko**
(MATUU PARISH-MACHAKOS DIOCESE)

**14th July 2023**

**Main Celebrant, Fr. John Njiru Provincial Delegate of Kenyan Delegation**
**at**
**St. Camillus Seminary Community Lang'ata –Karen**

**as from 10:00 AM**

## ENTRANCE

### TUMFANYIE SHANGWE

1.Njooni tumfanyie shangwe Mungu wetu .
Jiungeni wote tuimbe pamoja Kwa miondoko ya raha na kucheza
Kwa ngoma safi tamu na za midundiko
**Tumpigie) makofi makofi makofi (Tumpigie) makofi makofi makofi (Tumpigie) makofi makofi makofi makofi**
2.Bwana ametenda wema wa ajabu
Machozi ameyageuza vicheko Tumwimbie leo tumsifu yeye Tukipigapiga vifua kwa maringo
3. Tumpungieni mikono kwa madaha
Ajue kwamba leo tumefurahi Na shingo zinesenese kwa midundo
Mwili uyumbeyumbe kushoto kulia
4. Watoto nao wabebwe juu juu Wajue ya kwamba Mungu anawapenda Umati wote urukeruke juu Tusisite Mungu yu katikati yetu

### NALIFURAHI WALIPONAMBIA

1. Nalifurahi waliponambia twende nyumbani.X2 oh mwa bwana (wo lo lo lo lo) twende nyumbani.
**Twende twende nyumbani twende twende nyumbani twende nyumbani Njoni tuingie nyumbani mwake Bwana nyumbani oh Bwana mungu inapendeza mungu**.
2. Nyumba ya mungu ya kuabudiwa, njoni tukamwabudu x2
Nyumba ya mungu inayopendeza, kweli imejaa BarakaX2
3. Nyumba ya mungu ni yenye amani, pia ni yenye upendoX2
Tufurahie nyumbani ya mungu, kwani ni yenye furahaX2
4. Tucheze ngoma kinanda kinubi, gita kayamba na zeze tucheze ngoma.X2
Tumuimbie anayestahili, kwani ni mungu milele tumuimbie anayestahili.X2

### MAISHA YANGU

1. {Maisha yangu (yote) nakutolea (wewe) Ee Mungu wangu (Bwana) unipokee (kwako) }x2
**(Bwana maisha yangu yote nampa - Bwana maisha yangu yote nampa Bwana**
Nilivyo nanvyo vyote ni Mali ya -Bwana maisha yangu yote nampa Bwana) x2
2. {Ujana wangu (mimi), ulionipa (wewe) najitolea (kwako) kukuhudumu (wewe) } x2
3. {Uzee wangu (mimi), ulionipa (wewe) najitolea (kwako) kukuhudumu (wewe) } x2
4. {Nimeamua (mimi) na nyumba yangu (yote) kumtumikia (Mungu) milele yote (Bwana) }x2

## MASS

### BWANA UTUHURUMIE {SUBUKIA]

Bwana, Bwana, Bwana utuhurumie X2
Kristu utuhurumie, Kristu utuhurumie X2
Bwana, Bwana, Bwana utuhurumie X2

### UTUKUFU JUU KWA MUNGU

**{ Utukufu juu kwa Mungu, na Amani duniani, kwao watu wenye mapenzi, watu wenye mapenzi mema } X2**
1. Tunakusifu tunakuheshimu, twakuabudu tunakutukuza Twakushukuru kwa ajili yako, ya utukufu wako mkuu.
2. Ee Mungu baba ndiwe mfalme, Mfalme wa Mbinguni baba mwenyezi. Ee Yesu Kristu mwana wa pekee, mwanakondoo mwana wa Baba.
3. Uondoaye dhambi za watu tuhurumie tusikilize, Tuhurumie mwenye rehema maombi yetu uyapokee.
4. Uketiye kuume kwake, Mungu baba tuhurumie. Kwa kuwa ndiwe pekee yako, Pekee yako Mtakatifu.
5.Pamoja naye roho Mtakatifu, katika utukufu wake Anayeishi na kutawala, milele yote Amina.

### INJILI YAKE BWANA

1. Injili yake, injili yake Bwana aa aa inakuja kwetu sote tuipokee x2
**Injili ya Bwana iende mbele(iende) kwa mataifa yote, Mataifa wote wanangojea (injili ) neno hili la wokovu x2**





### SOMO WETU KAMILI-Basil Lukando

***Somo wetu Kamili (we Mtakatifu) somo wetu, ewe Kamili x2***

1. Twakuomba somo wetu, ***ee Kamili*** Mlinzi wa shirika letu, ***utuombee.***
2. Ewe msimamizi wetu,… Tumekuchagua wewe,…
3. Linda viongozi wetu,… Linda kazi ya kanisa…
4. Tupe afya ya wagonjwa,… Na amani ya rohoni,…
5. Wape moyo wa mapendo,… Wahudumu wa wagonjwa,…

### MTAKATIFU WE KAMILI-Lukando A. B

***(Mtakatifu we kamili) asante kwa kutulinda x2***
***Ulipokabidhiwa shirika hili, mbele yake Mungu kazi yako ni njema, miaka mingi leo umetulinda vyema x2.***

1. E-we Kamili, Mtakatifu sana, mlinzi wetu, Kamili:Utuombee.
2. Somo wa wagonjwa, Muuguzi mkuu, shujaa mkuu, Kamili: Utuombee.
3. Utusimamie, utuongoze, utuombee, kwa Mungu: Juu mbinguni.
4. Wauguzi wetu, uwape moyo, uwape afya, waweze: Kutoa tiba.

### OH KAMILO

***Mtakatifu Kamilo, oh Kamilo, oh Kamilo!***
***Sisi wanawako, Baba tunaomba; utuombee x2***

1. Katika shida tuombee, tuweze kumfuata Yesu.
2. Huduma zetu kwa wagonjwa, zipate nguvu ya Mungu.
3. Shida na taabu zinazidi, tuombee kwake Yesu.
4. Baada ya kazi zote ngumu, tufike sote mbinguni.

# PROGRAM

| | |
|---|---|
| 9:00 AM | Arrival |
| 9:30 AM | Preparation for Holy Mass |
| 10:00 AM | Mass and Temporal profession |
| 12:30 PM | Commissioning of Lay Camillians |
| 13:00 PM | Speeches & launching of Camillian Friends |
| 14:00 PM | Family Gathering and Lunch |

**Huyu ni Mama, Mama yake Yesu, anatuombea eeeh eeeh sikia, Anza na Mama, tembea na Mama, maliza na Mama ee ee Maria. Mama Maria yelele, Mama Maria yelele, Mama Maria yelele ee ee eeeh.**
2. Ninafarijika nikitaja lako ninajawa na furaha nikimba sifa zako ninashukuru ,
ma-alkia wa amani Maria msaada wa wakristu waridi lenye fumbo maria chombo-oo cha ibada
Tembea na mama injilisha na Mama,
Mama Maria, Mama Maria, Mama Maria, Mama Maria,
Tembea na mama injilisha na Mama,
Mama Maria, Mama Maria, Mama Maria, Mama Maria,
Tembea na mama injilisha na Mama,
Mama Maria, Mama Maria, Mama Maria, Mama Maria,
Tembea na mama injilisha na Mama,
Mama Maria, Mama Maria, Mama Maria, Mama Maria aah.
**Wewe Mama Maria mpendelevu Bikira Mama mwenye huruma,**
Tembea na mama injilisha na Mama,
**Mama wa shauri njema Maria wewe ni kimbilio cha wanyonge**,
Tembea na mama injilisha na Mama,
**Wewe kimbilio letu Bikira Mama mlinzi utuombee**,
Tembea na mama injilisha na Mama,
**Tunakulilia Mama Maria na sala zetu uzipokee**,
Tembea na mama injilisha na Mama,
Tembea na mama injilisha na Mama,
**Mama Maria, Mama Maria, Mama Maria, Mama Maria**,
Tembea na mama injilisha na Mama,
**Mama Maria, Mama Maria, Mama Maria, Mama Maria**,
Tembea na mama injilisha na Mama,
**Mama Maria, Mama Maria, Mama Maria, Mama Maria**,
Tembea na mama injilisha na Mama,
**Mama Maria, Mama Maria, Mama Maria, Mama Maria aah.**

## APEWE SIFA

{ Sifa na utukufu vyote ni kwa Mungu hee heee
Sifa na utukufu vyote ni kwa Mungu hee hee } X2
**{ Utukufu nakupa wewe, utukufu nakupa wewe, Sifa na heshima nakupa we, Ewe mwenyezi unaweza } X2**

1. Nguzo ya moto aliwasha, nilindwe usiku, Nayo ya wingu akashusha nipite mchana Nakumbuka mapito yote, niliyopitia, Nakumbuka na njia zote, nilizopitia
Tazama Mungu tazama wewe, Tazama Mungu tazama wewe Tazama Mungu tazama wewe unatimiza ahadi yako Tazama Mungu tazama wewe, (tazama Mungu ) ni mwaminifu Tazama Mungu tazama wewe unatimiza ahadi yako

Utukufu nakupa . . .
2. Jemedari mwenye maguvu, yule Goliathi, Akamlaza kwa kombeho, mkononi mwangu Nakumbuka alikemea, mawimbi ya maji, Nakumbuka yalimtii, nikafika ng'ambo Tazama Mungu tazama . . . Utukufu nakupa . . .
~ ~ ~
a) Bahari haiwezi kutuzuia - Tunatembea bila mitumbwi Na maji yanageuka kuwa ukuta - Mungu mwenyewe ni mtumbwi wetu tunavuka
b) Maana amesema tumfuate - Mizigo itulemeayo tukampe -
c) Muhimu tumwendee tukiamini - Na hata juu ya maji tutakanyagaa -
~ ~ ~
{ Alimkumbuka Daudi mtumishi wake Akamkweza akawavusha waisrael katika maji bila mitumbwi } X2
Apewe, apewe, apewe sifa kuu Mungu apewe, apewe, milele milele Apewe apewe, apewe sifa kuu Mungu apewe, apewe Sifa na utukufu vyote ni kwa Mungu hee hee





2. Injili yake, inaleta wokovu ee ee inakuja kwetu sote tuipokee x2
3. Injili yake, inaleta amani ee ee inakuja kwetu sote tuipokee x2
4. Injili yake, inafariji mioyo yetu inakuja kwetu sote tuipokee x2
5. Injili yake ,inaleta upendo ee ee inakuja kwetu sote tuipokee x2

## NASADIKI CENTINARY MASS

1. Nasadiki kwa Mungu mmoja - nisadiki Ndiye Baba yetu mwenyezi - nisadiki Mwumba mbingu pia dunia - nisadiki Nasadiki kwa Yesu Kristu - nasadiki Nisadiki (nasadiki) nasadiki nasadiki
2. Mwana wa pekee wa Mungu - Aliyezaliwa kwa Baba - Akapata mwili kwa Roho - Kazaliwa naye Bikira -
3. Kisha yeye kasulubiwa - Kwa amri ya Ponsio Pilato - Kwa ajili yetu kateswa - Akafa na akazikwa -
4. Kafufuka katika wafu - Kapaa juu Mbinguni - Ameketi kuume kwake - Mungu Baba yetu mwenyezi -
5. Ndipo atakapotokea - Kuhukumu wazima na wafu - Kwake Roho Mtakatifu - Kwa kanisa la Katoliki -
Ushirika wa watakatifu - Ondoleo la dhambi zetu - Nangojea fufuko wa miili - Na uzima wa milele -

## VOCATION

## Naskia Sauti

1. Nasikia sauti nzuri, kama ya malaika, Ni sauti toka mbinguni, sauti ya Mungu, Aniita mimi niende nikamtumikie, Anitume shambani mwake, nikavune yote.
**{ Umeniita, nimeitika wito, nakuja kwako leo, Najongea mbele zako, Bwana nipokee mimi, Niko tayari nimeyaacha yote najikabidhi kwako Unitume popote nami nitakwenda haraka } X2**
2. Ninaenda mimi naenda, ninaenda mwenyewe Ninaenda mbele za Bwana, sitarudi nyuma Ndugu zangu na marafiki mniache niende, Nikafanye kazi ya Bwana, nitakapotumwa.
3. Nilitazama moyo wako, moyo wako mwanangu Hata kabla hujazaliwa nilikutambua, Nilikuteua mapema, kati ya ndugu zako, Uwe kuhani wangu mimi, kuhani mkuu.
4. Shamba lake Bwana ni kubwa, na mavuno ni mengi, Wavunaji ndio wachache, nitakwenda mimi. Twakuomba sana ee Bwana, tupeleke shambani Tukavune mavuno yote, yaliyo tayari.
5. Uwe nami siku kwa siku, Bwana usiniache Unikinge na majaribu, nilinde daima, Nipeleke habari njema, ulimwenguni mwote, Watu wote wakutambue, wakugeukie.

## NIMTUME NANI

**Nimtume nani? Unitume mimi nitume Bwana x2 Nitakwenda kutangaza neno lako wewe mataifa wasikie wakufuate wewe, unitume mimi, nitume Bwana.**
1. Mkingali tumboni mwa mama zenu naliwatakasa, nalikuita ili uwe mtume wangu.
2. Mtakwenda kutangaza neno langu, msiogope kwa ajili ya hao.
3. Mimi katika mashaka na shida zao zote, mimi nitawafundisha mtakayosema

## SADAKA

## TUKATOE SADAKA

**(Twende wote tukatoe sadaka kwa bwana) Twende wote tukatoe sadaka kwa bwana) x2 (Twende----Twende tukatoe) x2 Twende wote tukatoe sadaka kwa bwana)**
1. Tukatoe mkate kiini cha ngano Twende tukatoe sadaka kwa bwana
2. Tukatoe divai tunda la mzabibu Twende tukatoe sadaka kwa bwana.
3. Tukatoe mazao ya mashamba yetu Twende tukatoe sadaka kwa bwana.
4. Nayo maisha yetu anatutakasa Twende tukatoe sadaka kwa bwana.
5. Vyote tulivyo navyo ndiye anatupa Twende tukatoe sadaka kwa bwana

## UPOKEE SADAKA YETU

1. Upokee sadaka yetu, twakutolea Baba
Upokee navyo vipaji, twakutolea Baba

**Pokea Baba zawadi X2 twakutolea Baba**
2. Upokee mkate wetu -
Upokee divai yetu
3. Upokee mazao yetu
Upokee na fedha zetu -
4. Nasi pia ni mali yako -
Tunatubu makosa yetu -
5. Upokee mioyo yetu -
Upokee na nafsi zetu -
6. Haya yote ni mali yako
Uyapokee kwa huruma -
7. Uviunge vipaji vyetu -
Na sadaka yake mwanao -
8. Usifiwe ewe mtukufu -
Kwa sadaka yake na yetu -
9. Utuhurumie wakosefu -
Tuletee baraka yako

## OFFERTORY

**NGAI NIARITURATHIMAGA**

**Ngai niariturathimaga, arathime mawira maitu**
**Arathime migunda itu, twamutegera na wendoX2**
Niegutuhe kiria giothe twamuhoya
Twamutegera na wendo
Niegutuhe buthi wa irio na mahiu
Twamutegera na wendo
Mawira maitu namo mone umithio
Twamutegera na wendo

Mirimu itu yothe niegutuhonia …………..
Atuehererie mogwati mawira – ini…………..
Atuhe thayu wa ngoro na wa mwiri …………

Riria twahanda agatuma tugethe ………….
Thuthi mbuca memenyi atwehererie ………….
Ng'aragu gwitu igutwika rugano …………….

**NGINYUKITIE**

Nginyuketie nguite rnugate na divai
niguo ngutegere Mwathani ciarnukire x2
**Ndahoya- ndayoya**
**Ndakuhoya- ngai ndahoya**
**Ngai unjitururie irathimo ciaku x2**

Moko-ini ma muguthinjiri amukira mbeca
gacunji kanini tu ka nyingi uhete x2

Nguite na moko magetha kuma migunda
Maciaro ma mimera iria tuhandaga x2

Kenio ni magetha maria ndiragutegera
ni uthaka na riri wa bururi uyu witu x2

Irathimo ciaku ni nyingi wee ngai wakwa
Unjituririe na itega riri riakwa x2

**MTAKATIFU (SUBUKIA)**

Mtakatifu Mtakatifu Mtakatifu Mungu wa majeshi
Mbingu na dunia zimejaa, zimejaa utukufu wako.
**Hosanna hosanna hosanna hosanna juu mbinguni**
Mbarikiwa anayekuja anayekuja kwa Jina la Bwana

**SING OF PEACE**

**Thayu wa Kristu uromuikurukira**
**Giai na thayu, na mugie naguo muno**
Kristu uomireire arekio akimera
Giai na thayu na mugie naguo muno
Athuri na inyui kristu aramwira . . .
Atumia na inyui kristu aramwira . . .
Ona inyui ciana kristu aramwira . . .
Riria mwarawara kristu aramwira . . .
Hindi ya thina kristu aramwira **. . .**

## COMMUNION

**UKARIMU WA BWANA**

1. Nani kati ya watawala wote wa falme wa dunia hii aliyewahi kuandaa karamu akaalika watu wote
**Ni nani kama Bwana Yesu mfalme wa mbingu na nchi anayetualika sote**
**kwenye karamu aliyoiandaa bali tuwe na moyo safi x2**
2. Sote tunaalikwa kushiriki kwenye karamu yake Bwana, tukiwa tajiri au masikini bali tuwe na moyo safi.
3. Ishara ya mapendo makubwa kwetu kutoka





kwake Bwana Yesu; kutoa mwili kutoa damu yake kuzishibisha Roho zetu
4. Ni fundisho kutoka kwake- Bwana tuonyeshe ukarimu kwa ndugu rafiki au majirani daima maishani mwetu

**AULAYE MWILI**

**Aulaye mwili wangu, na kuinywa damu yangu,Hukaa ndani yangu, nami hukaa ndani yake.**
1. Aulaye mwili wangu, na kuinywa damu yangu,Ana uzima wa milele.
2. Njoni enyi wenye njaa, njooni enyi wenye kiu,Njoni kwangu niwashibishe.
3. Aniaminiye mimi, na kushika nisemavyo,Nitamfufua siku ya mwisho.
4. Mlapo chakula hiki, mnywapo kinywaji hiki,Mwatangaza kifo cha Bwana.

**ENYI WAKRISTU WAPENZI**

**Enyi wakristu wapenzi njoni Bwana anatualika kwenye karamu x2**
**Kwanza ndugu tazama meza yake inavyopendeza yeye Bwana na wateule**
**wameizunguka meza yake Haya ndugu sismama nawe ushiriki x2**
1. Njoni Bwana atuita, meza yake sasa itayari ,haya simama nenda nawe ushiriki
2. Kama wewe wastahili fanya hima ukampokee ndicho chakula chenye uzima milele
3. Yeye anilaye mimi atakuwa na uzima mpya siku ya mwisho mimi nitamfufua
4. Yeye katuandalia masikini pia matajiri ukarimu gani Bwana Yesu alionao

## THANKSGIVING

**NIMRUDISHIE BWANA**

**Nimrudishie Bwana nini kwa ukarimu wote ,Alionitendea.nitakipokea kikombe cha wokovu,Nakulitangaza jina lake Bwana.**
1. Hakika Ina thamani machoni pake Bwana, inathamani kwake Bwana mauti yao
wacha Mungu wake.Ee Bwana hakika mimi ni mtumishi wako, mwana na mjakazi
wako ,umevifungua vifungo vyangu.
2. Nitakutolea dhabihu ya kushukuru, na kulitangaza jina la Bwana nitaziondoa

nadhiri zangu kwa Bwana naam mbele ya watu wake wote .

**NIMEONJA PENDO LAKO**

**1.**Nimeonja pendo lako, nimejua u mwema Nitakushukuru nitawainua wote wakusifu wewe Nitawaongoza vyema waimbe kwa furaha Nitakushukuru nitawainua wote wakusifu wewe.
**Ukarimu wako Bwana, na huruma yako wewe, Msamaha wako Bwana, na upole wako (wewe) Umenitendea wema usiopimika, Nitakushukuru nitawainua wote wakusifu wewe**
2. Kina mama simameni, piga vigelegele Na kina baba nyanyuka mkapige makofi
3. Watu wote nesanesa chezeni kwa furaha Inua mikono juu, mshangilieni Bwana
4. Watawa washangilie, makasisi waimbe Walei warukeruke, waseme aleluya
5. Vitambaa mikononi, vipeperushwe juu Na vichwa viyumbeyumbe kwa mwendo wa kuringa 6. Nitakushukuru mimi, na nyumba yangu yote - Nitayatangaza haya, maisha yangu yote -

## EXIT

**TAZAMENI NYOTA YA ASUBUHI**

**Tazameni nyota ya asubuhi, inang'aa hakika yapendeza ×2 nyota hiyo ni Mama Maria; njooni nyote tumshangilie Mama ×2**
1.Yeye ndiye bikira amini, yeye ndiye nyumba ya dhahabu
2.Yeye ndiye mlango wa mbingu, yeye ndiye chombo cha heshima
3.Yeye ndiye mama mpendelevu, yeye ndiye asiye na dhambi
4.Yeye ndiye bikira wa enzi, yeye ndiye mama wa huruma

**JINA MARIA – ZACHARIA GERALD**

1.Nitaimba sifa zako Ee Maria mama wake Mungu uliye kimbilio letu na ngao yetu
Nitataja jina lako mama Maria usiye na doa ni mama wa Mwokozi nitalisifu jina lako.
**(Mama Maria yelele, Mama Maria yelele, Mama Maria yelele ee ee eeeh.) x2**